jarida la kila mwezi

# NGURUMO ya mwandishi

TOLEO LA XXVII
DISEMBA MMXXIII



## YALIYOMO

**TAHARIRI**— 2023 Unaisha, Je; Umevuna ulichopanda?—Uk 02

**MWANDISHI WETU**—Rajab Hamis Said — Uk 03

**New In Town:** Ghubari La Kiza — uk 04

**PITIO LA VITABU**— Gamba la Nyoka (Ikisiri) 6—Uk 06

**MAKALA— SAIKOLOJIA**: Uwe na Kitu Cha Kujiringia —Uk 06 na 07

**RIWAYA:** Nilimuua Dada Niolewe Na Shemeji '12— uk 08 na 09

**MIAMBA WA AFRIKA:** Muammar Gaddafi '02'— Uk 10

**Sako kwa Bako– —**Uk 11

**RIWAYA:** —Kisasi cha Hisia '03'—Uk 12 na 13

**RIWAYA—** Cronoc 7 '9'- Uk 14 na 15

**YA KALE NI DHAHABU**: — Aladini na Wezi 40 '6'- Uk 16

**HABARI: Safari ya San Fransisco**– Uk 17

**SHUBAKA LA VITABU:** Zijue makta-ba 10 bora duniani '3'—Uk 18

**KITABU NILICHOSOMA:** Gifted Hands— Uk 19

**MATANGAZO: -** Uk20

**MALENGA WA KILEO—** Uk 21

**HABARI PICHA: -** Uk 22

**KUTOKA MAKTABA:** Miaka 62 ya Uhuru : Vituko Vya Uhuru**- '2'-**Uk 23

**ELIMU JAMII: Hakuna Mwanafunzi anayependa kufeli—**Uk 24 na 25

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0628124486**
**WhatsApp: +255 766974865**

**jamvilasimulizi@gmail.com**

# TAHARIRI: 2023 Unaisha, Je, umevuna ulichopanda?

Wasalaam,

Napenda kukusalimuni ninyi nyote wapenzi na wasomaji wa jarida hili. Najua kila mmoja yupo kwenye haihai za kuumaliza mwaka huku bado matumbo yetu yakiwa yamejaa pilau na mapochopocho ya Krismas. Oh tumshukuru Mungu kwa wema wake kwani yote hayo ni mapenzi yake. Wangapi wameshindwa kuuona mwaka huu mpya? Wapo ambao uhai wao umepotea dakika moja tu kabla ya mwaka mpya kuingia. Yote hiyo ni mipango ya Mola.

Lakini nini maana ya kufurahia kuumzaliza mwaka na ipi maana ya kufutahia kuuanza mwaka? Je kwako wewe yana maana gani? Kila mtu ana jibu lake. Yupo anayefurahi tu kwa kuwa kafika mwaka mwingine. Yupo anayefurahi kwa kuwa mipango aliyoipanga mwaka huu unaiokwisha ameitimiza kwa asilimia kubwa. Yupo anayefurahi tu akisema kwamba mwaka uliopita ulikuwa na mikosi.

Yote ni sahihi, inategemea tu upo kwenye kundi lipi. Lakini kumbuka kwanba kuwepo kwa mpangilio wa miaka ni makusudi mazima ya kukusaidia wewe na mimi kupanga taratibu za maisha yetu. Yaani hapa mpaka hapa nitafaya nini na pale mpaka pale nitafanya nini. Kalenda na mpangilio wa miezi na tarehe vipo na vimewekwa ili viku-saidie katika hilo. Je umefanya hivyo?

Mwaka 2023 umeisha, ulipanga mipango gani? Umeitimiza yote? Au asilimia Fulani? Au imeshindikana kabisa?

Kama umeitimiza yote, hongera na mshukuru Mungu kwa ku-kusimamia maana si kwa nguvu zako. Na kama umetimiza kwa asilimia fulani pia hongera na mshukuru Mungu. Kama yote uliyoyapanga hayajatimia, usikate tama, huu ni mwaka mwingine, kaa chini, weka mi-pango upya, jitathmini ulikosea wapi na amua kurekebisha makosa hayo, kisha endelea kupambana kwa mwaka huu.

Hatutakiwi kuishi duniani bila malengo. Tazama miti ya matun-da, kila mwaka lazima ikupe matunda si kwa muda wote bali kwa mwe-zi maalum huku ikipishana na aina nyingine ya matunda. Hutakiwi ku-pata matunda yote kwa wakati mmoja, hapana. Bali miezi kumi na mbi-li ya mwaka miti itakupa matunda kadiri ya wakati na majira ya mwaka.

Je wewe si mti wa matunda mbele ya jamii? Je mwaka huu umevuna ulichopanda? Pambana, usiogope.

Nakutakia heri nyingi na neema za Mungu kwa mwaka huu mpya wa 2024.

© Richard MWAMBE

# MWANDISHI WETU: RAJAB HAMIS SAID




Naitwa Rajab Hamis Said.

Ni muhitimu wa chuo, nikiwa nimetahasusi katika ualimu wa masomo ya lugha (Kichina & English).

Mapenzi yangu makubwa ya kusoma vitabu, hasa riwaya za Kiswahili tangu nilipokuwa mdogo kabisa, ndiyo yaliyopelekea nikigundue kipaji changu cha uandishi. Mwaka 2014 ndio mwaka nilioanza kuandika. Nilikuwa nikiandika kwenye madaftari ya shule niliyokuwa nikiyatumia kama 'rafu.' Mwaka 2019, ndio mwaka niliopata ujasiri wa kuanza kutuma hadithi mtandaoni, kwenye mtandao wa Facebook. Hadithi yangu ya kwanza ikiwa imechanganya tanzu mbalimbali ndani yake; Ilikuwa na historia, sayansi pamoja na nguvu za giza kidogo!

Mpaka sasa nimeandika kazi si chini ya kumi, na nimechapa kitabu kimoja tu, ambacho ni MONEY BANK. Kitabu hiki kwa mara ya kwanza kabisa kimeanza kusomwa mwaka jana Disemba. Hii ndiyo kazi ambayo unaweza kuipata kwa sasa! Hata hivyo nasikitika kuwa madukani nakala zimekwisha, isipokuwa kwa wakala mmoja tu wa Moshi. Hivyo kama ukikihitaji kitabu hiki kwa sasa, kwa wakazi wa Moshi na Arusha nakala zipo, ila nje ya hapo unaweza kuweka oda kwani vitabu vitachapwa tena hivi karibuni!

Kazi zingine ambazo unaweza kuzisoma kwa sasa kutoka kwangu, ni riwaya za kisaikolojia ambazo ni JAMILA NA MBWA KICHAA, pamoja na JAMILA NA KICHAA CHA MBWA. Zote hizi bado zipo kwa mtindo wa nakala laini.

Kwa wasomaji wa fasihi ya kiswahili, kwanza napenda kuwashukuru kwa moyo wenu mkubwa ambao unaendelea kutufanya waandishi tusikate tamaa. Naweza kusema kuwa bila nyie, basi hakutokuwa na waandishi.

Fasihi ya Kiswahili ina wapenzi wengi, japo nikiri kuwa bado inahitajika nguvu yenu kubwa wasomaji kwa kushirikiana na watunzi, ili tuzidi kwenda mbali zaidi. Safari bado ni ndefu, kwetu sote, waandishi chipukizi na wale ambao tayari wametutangulia hatua nyingi mbele pamoja na wakongwe. Mungu awape moyo huohuo wa kuendelea kutushika mkono kwa maendeleo ya fasihi na lugha yetu hii adhimu kwa ujumla, izidi kupaa kimataifa!

Mwisho natoa ahsante nyingi kwako AMATA RIC, kwa kunipa wasaa huu wa kukikalia kilinge hiki kwa siku ya leo! Nakiri huu ni upendeleo mkubwa kwangu! Mungu akuzidishie na akufungulie kwa kila unalolihitajia!

## Penda kusoma vitabu

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

**Faida za kusoma vitabu:**

- Msisimko wa Akili
- Kupunguza Msongo wa Mawazo
- Kuongeza Ujuzi wa mambo mbalimbali
- Kuongeza Msamiati
- Huboresha Uwezo wa Kukumbuka
- Hukupa Uwezo Mkubwa wa kuchambua na kufikiri
- Huboresha Mtazamo na Umakini

Kwa mawasiliano na mimi, kwa ajili ya ushauri au lolote lile, kwa mtu au msomaji yeyote, unaweza kunicheki WhatsApp kwa namba hii:

**0655910113.**

Ahsante!

## NEW IN TOWN

Wema Akiba
Ghubari la Kiza ni mkusanyiko wa Riwaya fupi tatu zenye mafunzo ya kipekee sana katika jamii. Sasa kuna hiyo Riwaya ya pili inaitwa Wema Akiba, yaani kuna watu wamefanya wema uliovuka kiwango na matunda yake wakayaona hapa hapa duniani!

Ilikuwa hivi...
Wavulana watatu waliondoka kwenye nchi yao iitwayo Rausi kwenda Tauredi kutafuta nafuu ya maisha. Wakati huo Tauredi ilikuwa ikivuma sana kwa kuwa nchi yenye maisha bora na neema za kila namna.
Wavulana hawa walitembea kwa miguu. Wakati ule hapakuwa na motokaa. Lakini pia hawakuwa na uwezo wa kumiliki farasi ama ngamia. Tauredi iko mbali sana kutoka Rausi. Kwa miguu ni mwendo wa miezi mitatu na nusu. Si hivyo tu Tauredi haifikiki kirahisi. Njiani kuna mapori na misitu ya kutisha. Kama ni mastakimu basi si zaidi ya vijiji viwili. Fauka na hayo kuna wanyama wakali. Baadhi ya watu waliojaribu kwenda huko wamekutana na misukosuko tolatola huku wengine wakipotea fefefe!

Safarini wavulana hawa jamali wanakumbana na kila aina ya kadhia zikiwemo maradhi, kiu na njaa. Kwao si kitu kuliko azma yao ya kufika Tauredi. Ingawa walionywa sana na watu wazima wasiende huko ila walitia pamba masikioni. Waliweka nadhiri lazima wafike Tauredi.

Wakiwa wamebakiza mawiki machache kuisogelea Tauredi mvua kali ikawakumba wakiwa njiani. Wakaona cha kufia nini? Ngoja tutafute pahala pa kujihifadhi. Watatu hawa wakaingia pangoni. Mvua nayo haikuacha hadi siku ya pili. Walipotaka kutoka wakakumbana na mkasa wa aina yake ambao ndio unaibua lengo la simulizi hii!


Ni nini hicho hasa?
Walikuta ule mlango wa kuingilia pangoni haupo! Jabali limeporomoka kutoka nyanda za juu na kuuzinga mdomo wote wa pango. Ikawalazimu kuingia kazini kulisukuma jiwe ili liondoke na waweze kutoka. Ikawa sukuma, sukuma na wewe! Jabali si tu halikusogea bali hata kutikisika halikutikisika! Takribani saa nne za kuminyana na jiwe hazikuzaa matunda na mwishowe wakaishiwa nguvu na kujitupa chini wakipoteza rajua. Wakiwa wametehemu kukingoja kifo ndipo mwenzao akapata wazo. Akawaambia wenzie kila mmoja kwa wakati wake amkabili Mwenyezi Mungu kisha ataje wema mmoja tu wenye nguvu ambao amewahi kuufanya na kupitia wema huo amwombe Mungu lile jiwe lisogee. Wenzie wakamshangaa sana. Vipi jambo hilo liwezekane? Yaani mathalani leo uwasaidie wana yatima kwa kuwapa chakula halafu kupitia wema huo umwombe Mungu uokote burungutu la pesa!

Inawezekana?

Je ni wema gani mzito walioufanya hawa vijana? Wema ambao ulimshawishi Muumba aliamuru jiwe lipishe? Wema ambao pengine nawe waweza kujifunza kutoka kwao.

Fuatana na mwandishi Salim Hussein Ng'anzi katika kitabu hiki cha **Ghubari la Kiza** kujua mengi.

**Tsh. 10,000/=**
**0719 867 477**



# KITABU: GAMBA LA NYOKA –Ikisiri (6)

**Ikisiri hii imeandikwa na Mwenda Mbatia, nasi tumeiweka hapa kwa msaada wa mtandao ili wanafasihi mjifunze zaidi.**

Lakini tabia na mienendo yake ni kinyume cha matarajio haya. Mbali na sifa zilizotajwa hapo juu, mhusika huyu ni mdanganyifu mkubwa. Inakuja kugunduliwa hatimaye kwamba Emptyhead sio padri bali jasusi wa shirika la upelelezi la CIA. Kazi yake hasa ilikuwa ni kuvuruga Ujamaa nchini Tanzania kwa niaba ya serikali ya Marekani ambayo ilichukia siasa za aina hii kwa sababu ilizihusisha na Ukomunisti.

Mfano mwingine wa kinaya cha hali unahusiana na vifo vya Padri Madevu na mpenzi wake Mama Tinda. Mambosasa ndiye anayepanga kifo cha Padri Madevu ambaye ni adui wake mkubwa. Anamtumia mpenzi wake na baadaye mke wake, Tinda, kutekeleza mpango wake ambao unahusu kumtilia Padri Madevu sumu katika chakula. Mpango huu unatekelezwa Padri Madevu anapomtembelea Mama Tinda nyumbani kwake kama kawaida. Kwa bahati mbaya, mamake Tinda pia anakula chakula ambacho kilidhamiriwa kuliwa na Padri Madevu peke yake. Kesho yake, wote wawili wanakutwa wakiwa wamekufa. Tunaelezwa kama ifuatavyo: "Mama Tinda na Padri Madevu walikuwa wamekauka hali wamekumbatiana. Ilikuwa aibu ya mwaka." (uk. 81) Hivyo ndivyo Tinda anavyosababisha kifo cha mamake bila kudhamiria.


**4.0 Mzee Chilongo**

Mhusika huyu ni kiwakilishi cha Watanzania ambao wamedhibitiwa na utamaduni wa kijadi kiasi kwamba hawataki mabadiliko hivyo wanapinga Ujamaa ambao unahusishwa na ujenzi wa jamii mpya. Vitendo na matamshi yake yamewasilishwa kwa ucheshi mkubwa kwa hivyo ni wa kusisimua na wakati huo huo kuufichua udhaifu wa mhusika huyu. Sifa kuu ya Mzee Chilongo ni kuchukia kwake mabadiliko na kujitolea kwake kupingana nayo. Lakini jitihada zake zinachekesha kwa sababu ni wazi kwamba katika muktadha ulio ndani ya riwaya haziwezi kufaulu. Mbinu kadha za kitashtiti zimetumiwa kuushambulia uhafidhina wake.

Mfano mmoja wa jitihada za Mzee Chilongo kupigana na mabadiliko unahusiana na tukio la wanakijiji wa Kisole kuamua kukataa kuhamishiwa kwenye kijiji kipya. Hivyo, wanaume wote wanajificha porini ili kupambana na wanamgambo wa serikali wanaokuja kuwahamisha. Mzee Chilongo ni mmojawapo wa wanaume wanaowa- shambulia wanamgambo. Anajitokeza kuwa hodari katika matumizi ya silaha za kiasili kama vile uta na mishale. Baada ya mapambano, anawaeleza wenzake jinsi alivyomfuma mshale mwanamgambo:

*Nilimshika vizuri 'sina-huruma' jina la mshale wangu, kisha nikavuta. nikalenga barabara sikio la kongoni wangu mnono. Nilipouacha, mshale ulikwenda kama upepo, nao haukuvunja ahadi yake. Ulitua vizuri pale pale nilipoutuma, ukaziba lile tundu lenye kiburi lililokataa kusikia kilio chetu. Mara moja nilimwona huyo kongoni anarukaruka kama beberu ililonusa matako ya mbuzi jike (uk. 30).*

Ucheshi wa kifungu hiki umerutubishwa na mbinu nyingine kadha za kimtindo ambazo zinaleta athari ya msisitizo na udhahiri. Kwa mfano, kuna tashihisi inayotokana




na Mzee Chilongo kuuzungumzia mshale wake kana kwamba ni binadamu. Sikio pia linahusishwa kwa kurejelewa kama lenye kiburi. Pia, kuna sitiari inayotokana na ulinganishaji wa mwanamgambo na korongo mnono. Hii inaleta picha ya windo lenye thamani kubwa. Pia, kuna tashibihi ya kuchekesha mwishoni ambapo athari ya windo kufumwa na mshale sikioni inamithilishwa na afanyavyo beberu anaponusa sehemu za uzazi za mbuzi jike. Mifano hii inathibitisha kwamba mtindo huu, hasa ucheshi, kinaya, chuku na tabaini.

*Itaendelea...*

# UWE NA KITU CHA KUJIRINGIA

**Madame Neema Mbilinyi Mgao.**

**WhatsApp no.**
**+255 746 139 654.**

**Simu:**
**+255 763 013 206.**



**UWE NA KITU CHA KUJIRINGIA.**

Binafsi namshukuru Mungu kwa mwaka 2023, ni mwaka ambao alinikutanisha na wewe na nikaweza kusema na Saikolojia yako kwa namna Mungu alivyoniwezesha. Ukurasa huu uliniwezesha kutoa makala ya kisaikolojia kila mwezi na nimshukuru Mungu kuna watu wameponywa majeraha ya nafsi zao kwa namna ya kipekee kadri ya vile alivyojiandaa kupokea. Na matokeo chanya yametokea kulingana na kila mtu na uhitaji wake nyakati husika.

Hongera saana kwa kuumaliza mwaka 2023, hadi kufikia leo ni dhahiri kuwa umehimili maumivu mengi mabaya na pengine yalitaka kutoka na nafasi ya utulivu katika akili na fikra zako. Pole kwa mikiki mikiki yoote uliyokutana nayo kwa mwaka mzima na hongera kwa kuishinda mpaka sasa upo imara. Leo tuzungumze kuhusiana na kujiringia.

Nini maana ya kujiringia?

Kujiringia ni neno nililoona linafaa leo kulitumia, kujiringia linatokana na neno "ringa" ambalo huleta maana ya kujivunia hali uliyonayo, pengine uzuri, au mafanikio. Unaweza kukuta anapita mwanadada mbele ya kadamnasi ya wanaume na ukasikia *"aaahhh,huyu dada ni mzuri jamani, na anaringa vibaya mno"*, umeona neno 'ringa' lilivyotumika. Hivyo kuringa ni kujivunia jambo fulani iwe uzuri au hali fulani uliyonayo. Kwa maana hiyo, neno kujiringia maana yake ni kujivunia.

Kujiringia kisaikolojia ni nini?

Kama tulivyoona maana ya kujiringia kuwa ni kujivunia, basi kisaikolojia hali ya kujiringia huwa ni kama tiba ya kisaikolojia. Mtu yeyote anaweza kupitia hali ya matatizo makubwa kiasi ikapelekea pengine kupuuzwa au kuonekana sio kitu, na bahati mbaya sana, tunaishi kwenye jamii ambayo haifichi hali zao pale wanapoonesha hali fulani kwa wengine, hasa chuki. Mtu yuko radhi akuoneshe kukuchukia kuliko kukupenda, mtu yupo radhi na ni rahisi akabeza juhudi za mwingine kuliko kumuonesha ushirikiano, hali kama hiyo ya kushuhudia kuchukiwa hupelekea mtu pengine kujichukia na yeye au kujidharau.

Ni kama mtu aliyetoka kuumwa sana, mwili ukamporomoka (akakonda), hata ikapelekea kuwa wengine wanapokutana nae au wanapomuona waoneshe dhahiri kuwa mtu yule ameisha mwili, hali hiyo mtu anapoishuhudia nyusoni mwa watu hupelekea mtu husika kupokea ule mshangao wao na kumfanya mtu ajidharau. Au mtu yule pengine aliwahi kuishi maisha ya ukwasi (hali ya maisha mazuri) nyakati fulani, halafu pengine akapata matatizo katika mfumo wa maisha yake na impelekee ghafra kupitia ukata (hali ya maisha magumu), vile jamii inapomuonesha kumshangaa na kumcheka pengine ndivyo nae anapoyapokea yale maumivu ya kubezwa na kuanza kujidharau.

Akili ya mwanadamu au ndani ya fikra zake ipo hali mfano wa mpangilio wa mambo au matukio yote kwa maandishi na kuwa kama kumbukumbu katika kichwa chake, licha ya kuhifadhi matukio mbalimbali pia mwanadamu amejihifadhi yeye mwenyewe na maisha yake ndani ya kichwa chake. Saikolojia ya mtu huenda kwa mapokeo kadri ya matukio yanavyomtokea, kama mtu akipita mbele za watu na watu wakacheka ni dhahiri mtu huyo atahisi kuchekwa yeye na kwakua akili yake imemsemesha yule wa ndani yake (kuna yule wewe ndani yako) basi mwili utapokea ile hali ya kuchekwa na ni wazi kuwa pengine mwendo utabadilika au pengine hata kujikwaa.

Uwe na cha kujiringia, ni sawa jamii inawezekana imekubeza, ila hakikisha uwe na cha kujiringia,

# -SAIKOLOJIA-
# UWE NA KITU CHA KUJIRINGIA

na hicho cha kujiringia ukikipata usikiachie, kisambaze ndani ya akili yako na kitumie kukupa nguvu katika mwili mzima.

Pengine ulikua mnene na mwenye afya nzuri sana, ghafra ukaumwa na kupelekea mwili kuisha, pata kitu kimoja tu kitakachokufanya ujiringie, pengine una macho mazuri, au pengine mikono yako milaini (nyororo) basi moja kwa moja peleka upekee huo katika akili yako na uutumie katika kukupa nguvu ya mwili wako mzima, iambie akili yako kuwa "*hakuna mwenye macho mazuri kama mimi*" au "*miguu yangu haina gaga*( mpasuko wa mguu)". Pata hata kitu kimoja tu cha wewe kujivunia nacho, cha wewe kujiringia katika mfumo wa maisha yako.

Katika mfumo wa akili yako, gundua kuwa ni kitu gani cha upekee kwako,yaani kile kitu ambacho mwingine hana, weka kitu kimoja au hata viwili ambavyo vitakuonnesha upekee wako. Gundua upekee wa maisha yako pia, halafu moja kwa moja peleka upekee huo katika "files" za akilini mwako.

Ukishaugundua upekee wako tumia huo huo upekee kujiringia ili usiidhuru akili yako kwa kuumiza fikra zako. Ringia walau kitu kimoja tu ili kikuinue katika anguko hilo ambalo ni mpito kwako, ama la kiuchumi, au la kiafya.

Hakuna mtu mwingine anaeweza kujivunia au kuringia uwepo wako zaidi ya wewe mwenyewe utakavyofanya, mtu hawezi sema "*najivunia macho ya fulani*" sasa ajivunie macho ya mwingine yamsaidie nini?, au aseme "*najivunia biashara ya fulani*" ili iwe nini. Kwa mantiki hiyo utagundua kuwa upekee wa mtu ni kwa ajili ya mtu mwenyewe, ni kwa manufaa ya mtu binafsi ambayo anapaswa kuyaringia yeye binafsi.

Uwe na cha kujiringia, ukikipata usikiachie kisambaze ndani ya akili,mwili wako hadi kupelekea wewe kupata nguvu zaidi na sio kukata tamaa. Ilinde akili na Saikolojia yako kwa kujisemesha upekee wako na wengine na kujiringia katika upekee huo.

Asante kwa kuwa nami katika makala hii ya Saikolojia kwa kipindi chote cha mwaka 2023, katika kipindi hicho chote cha mwaka, kila mwezi kumetoka makala moja ya kisaikolojia, hivyo hakikisha unazo makala zote 12, kama hauna nitumie ujumbe kupitia WhatsApp no. +255 746 139 654. Karibu sana.

Utulivu wa akili yako ndiyo furaha yangu. Tuuanze mwaka 2024 tukiwa watulivu.
Asante.

Madame Neema Mbilinyi Mgao.
What's app no. +255 746 139 654.
Simu:+255 763 013 206.

Ngurumo ya Mwandishi, tunakushukuru sana kwa makala hizi za kisaikolojia. Ni hakika watu wengi wameponywa kwa kusoma makala hizi. Hivyo basi wewe msomajio, kama ulivyosaidiwa na makala hizi, hakikisha na rafiki yako anasaidiwa pia, sambaza jarida hili kwa wote uwapendao ili nao wapate kuponywa.

Madame Neema Mbilinyi yupo kwa ajili yako, mpigie au mwandikie ujumbe WahatApp kwa maswali na ushauri zaidi juu ya matatizo na ushauri wa kisaikolojia. Nikutakie heri ya mwaka mpya.

***Inatoka Ukurasa wa 17***

Lilian Mbaga (na mfasiri wake Dkt. Uta Reusterd) kwenye mkusanyiko huo wa No Edges, ni jambo kuntu mno. Ninaamini, safari yangu hii ya kuja kuwatembelea hapa Marekani inafungua njia muhimu kwa simulizi za Kitanzania. Ninaamini, safari hii inachonga barabara itumiwe na waandishi wenzangu wengi. Tanzania ina utajiri wa fasihi ya Kiswahili. Ambayo, kama nilivyowaambia watu kwenye hafla ya jana, ni wa kipekee mno ukisawiri mambo kedekede kwenye nyanja zote za maisha.
Kuna raha sana kuzuru jiji kubwa la San Francisco. Ila raha zaidi, kupata wasaa wa kukuandikia haya.
Hadi wakati mwingine.

*Fadhy Mtanga,*
*Kimpton Alton Hotel,*
*2700 Jones Street,*
*San Francisco, California.*
*15 Desemba 2023.*

# HADITHI: NILIMUUA DADA NIOLEWE NA SHEMEJI-12



Na. Makoleko Kalibonge

**Hayakuwa katika mpangilio na nyasi zilikuwa nyingi. Taratibu nilisogelea geti nikagonga. Sikupata jibu. Niligonga tena na tena na tena. Hapakuwa na dalili ya kuwa na mtu ndani wala mlinzi hakuwepo.**

Sikutaka kuamini kuwa hapakuwa na mtu kweli. Nilichungulia kupitia uwazi mdogo uliopo katika geti, nikaliona gari la shemeji. Nikajiambia kwamba yuko ndani kwani hawezi kuondoka bila gari. Niliendelea kugonga kwa nguvu zote bila mafanikio. Nilikata tamaa ya kumpata mtu ndani. Nilibaki nimesimama getini nikiwa nimechoka sana. Nilijilaumu kwenda kwa mtu bila kutoa taarifa. Sikuwa na jinsi ya kufanya zaidi ya kumpigia simu. Wakati naugeuza mkoba wangu nitoe simu nikasikia mlango unafunguliwa. Nilishtuka kukutana sako kwa bako na shemeji. Alikuwa anatoka. Mkononi alibeba kikapu kidogo ambacho ndani yake mulikuwa na hotpot.
Aliponiona naye alishtuka. Alipigwa na bumbuwazi asiamini alichokiona mbele yake.

"He! umefika muda mwingi?" Aliniuliza.

"Hapana! Nimefika muda huu. Nilikuwa nataka nikupigie simu nikujulishe kama niko nje. Ya wapi na makapu?"

"Naingia hapo restaurant. Si wajua leo Jumapili niko home tu sasa nimeona bora nichukue chakula nikae nacho ndani," alisema shemeji. Nilimhurumia sana. Kwa hakika alitaabika kupata chakula. Angalikuwepo mkewe asingalisumbuka namna hii kwenda huku na huko kutafuta chakula.

"Karibu ndani." Akanikaribisha huku akifungua zaidi geti. Aliniongoza kuingia ndani. Moja kwa moja hadi sebuleni. Nilichokikuta hapo ni aibu kukisimulia. Sebuleni palikuwa zaidi ya nje au jalala. Kila kitu kilikuwa ovyo – hakuna kitu kilichokaa sehemu yake. Nguo zote zilihamia sebuleni. Ilionesha kuwa alikuwa analala hapo. Shuka zilikuwa hapo, nguo za ndani, suruali, mashati na viatu vyote vilikuwa hapo. Wakati wote alikuwa mwenye wasiwasi. Alinikaribisha niketi kwenye moja ya sofa ambalo halikuwa na makorokoro.
Alizikusanya nguo kisha aliingia nazo chumbani. Sikutaka kukaa nilipokaribishwa. Nilisimama nikiyatembeza macho kuyasawiri zaidi mazingira. Mazingira yalikuwa ovyo. Taratibu nilijivuta kuzunguka mule ndani. Nilipotoka sebuleni niliingia moja kwa moja jikoni. Huko ndiyo kulikuwa hatari tupu; vumbi kila mahala, tandabui zilitanda na kombamwiko walisambaa kila kona.

Nilipotosheka kuzunguka mule ndani nilirudi sebuleni. Nilimkuta shemeji amekaa kwenye kiti nyuma ya meza ndogo. Alikuwa mwenye mawazo na aibu kubwa. Aliponiona alikurupuka kama aliyeshtuswa na kitu akasimama. Aliniangalia usoni nikaona aibu. Kitu fulani kilipita moyoni mwangu. Hivyo niliyapindua macho nikaangalia chini.
"Mi' natoka naenda kuchukua chakula. Nikuletee chakula gani?" Aliniuliza.

"Mi' sili chakula cha mgahawani," nilimjibu huku nikisugua vidole. Mwili wangu ulikuwa na joto la ajabu.
"Kwa hiyo utakula nini? Pia hakuna mtu wa kukupikia," alisema shemeji kwa sauti ya chini iliyojaa huruma. Nilitulia nikizungusha akili. Nilitaka kumwambia akanunue mahitaji nipike. Wazo dogo lilinijia. Nilikurupuka nikaingia tena jikoni. Niliendea friji nikalifungua. Humo nikakutana na makorokoro mengi ya kufaa kupika. Nilirudi haraka sebuleni. Bado shemeji alikuwa vilevile kama nilivyomuacha.

"N'tapika," nilimwambia. Hapakuwa na maongezi tena. Niliingia jikoni kuanza kutayarisha chakula. Na, kwa kuwa muda uliruhusu, nilipomaliza kupika nilifanya usafi. Haikuwa kazi rahisi. Nilijitahidi kufanya usafi hata palionekana kama kuna mwanamke. Nilipomaliza shughuli zote niliandaa chakula mezani. Kisha nilimuamsha shemeji aliyezama usingizini. Tulijumuika pamoja mezani kula chakula. Tulipomaliza kula zilifuata stori za hapa na pale. Ilipotimu saa kumi alasiri, tulikwenda ufukweni. Giza lilipoingia shemeji alinirudisha nyumbani.

# HADITHI: NILIMUUA DADA NIOLEWE NA SHEMEJI—12

Ukaribu wangu na shemeji ulinipa matumaini ya kufanikisha azma yangu. Alinipigia simu kila alipohitaji nami nilifanya hivyo bila pingamizi. Tulitaniana na kufurahi.

Hakika nilifarijika sana. Mapenzi yangu kwake yaliongezeka mara dufu nikashindwa kujizuia.
"Mama nahitaji kuongea na wewe." Ilikuwa siku moja jioni baada ya kurudi kutoka stationary.
"Kuna nini tena kipenzi, mbona wanitisha?"
"Hapana mama sikutishi. Kawaida tu," nilimtoa wasiwasi.
"Mh! Haya." Mama alinijia nilipo akakaa karibu yangu.
"Haya, mrembo wangu niambie una nini?" Nilikosa ujasiri wa kumwambia kusudi langu. Nilijuta kwa nini nilimwambia vile. Sikujua nianzie wapi kwani sikufahamu atalipokeaje ninalotaka kumwambia. Nilibaki kimya nikitizama chini kwa aibu.

"Nakusikiliza mwanangu."
"Baba yuko wapi?"
"Amekwenda barabarani huko, vipi unamtaka?"
"Hapana. Nimeuliza tu."
"Haya niambie."
"Nampenda shemeji," nilisema bila hofu. Sikutaka kumficha jinsi nilivyojisikia kwa shemeji. Nilimsimulia juu ya ukaribu wetu na kitu ninachokitaka kwake. Nilipomaliza kumwambia aliniuliza,
"Umemwambia mwenyewe?"
"Hapana mama. sijamwambia."
"Sawa nimekuelewa. Nitamwambia baba yako halafu tutajua tunafanyaje." Mama alinitia moyo. Matumaini yangu kwamba atanisaidia katika hili yalikuwa makubwa baada ya kumsimulia.
Sijui waliongea muda gani na baba. Usiku uliofuata baba aliniita. Aliniuliza juu ya niliyomwambia. Nilimthibitishia na kumhakikishia kuwa nampenda sana. Ningefurahi zaidi kama nitafunga naye ndoa. Tupozungumza kwa kitambo aliruhusu nikalale naye aliiingia chumbani kwake.

Siku tatu baadaye nyumbani palifika mgeni. Alikuwa baba yake shemeji ambaye alipigiwa simu na baba. Alipofika kazi ilikuwa moja tu kumwambia nilichomwambia mama, halafu baba.
"Sawa mzee mwenzangu. Nimekusikia na nimekuelewa. Nadhani leo nitamwita ili nizungumze naye. Nitakupa taarifa baada ya kuwasiliana naye." Baba yake shemeji alisema na kuondoka baada ya maongezi ya muda mrefu.

*** * ***

Unaweza usiamini. Nilitegemea ugumu na upinzani mkubwa kutoka kwa shemeji katika hilo. Ajabu ilionesha kwamba alikuwa anasubiriwa mtu wa kuanza kusema. Namshukuru Mwenyezi Mungu kile nilichokiomba usiku na mchana kilitimia. Baada ya darasa kutoka kwa baba na mama yake na ndugu wengine, shemeji alikubali ombi langu la kunioa. Nilifurahi sana ilipokuja barua ya posa. Haraka vikao vya harusi vilianza kushika hatamu. Moyo wangu haukuwa tena na huzuni ya kumuua dada. Nilishangilia ushindi kabla goli la pili halijaingia. Nilijipongeza kwa kutimiza azma yangu. Haya mapenzi yaachwe kama yalivyo. Siku ya ndoa ilipangwa. Taarifa zilisambazwa kwa ndugu jamaa na marafiki wa pande zote mbili. Dada mkubwa alipewa taarifa na kaka alipewa taarifa pia. Hata hivyo nilihisi nimetengwa na sipendwi.

Japo wawili hao walipewa taarifa ya kuolewa kwangu walitoa udhuru wa kutofika. Dada mkubwa alidai amebanwa sana na kazi hivyo hatohudhuria ndoa ila alitoa baraka zote. Kaka alisema tarehe hiyo itamkuta Bara Arabu kutiliana mkataba wa ushirikiano baina ya kampuni anayofanyia kazi na kampuni moja ya huko. Hivyo kufika kwenye ndoa ilikuwa ndoto. Naye pia alisema ametoa baraka zake zote na kuahidi akitoka huko kabla ya kwenda Nigeria atakuja.

Haikuishia hapo, pigo lingine ni kutoka kwa rafiki yake dada marehemu. Nilimpelekea taarifa za kuolewa kwangu na shemeji. Siku mbili kabla ya ndoa ndiyo ilikuwa siku ya kujifungua kwake, hivyo haikuwa rahisi kuhudhuria. Nyumbani penyewe ilikuwa balaa tupu, shangazi alikuwa hospitali amelazwa akiugua kisukari. Kutokana na mambo hayo nilijua haikuwa halali yangu kuolewa na shemeji. Watu wote muhimu niliowategema hakuna hata mmoja aliyehudhuria zaidi ya baba na mama.

Kwa upande wake shemeji ilikuwa kama kituko. Hakuonekana mama yake wala shangazi yake. Kaka yake alikuja asubuhi halafu aliondoka baada ya kupigiwa simu akitakiwa kuwa Arusha saa saba ya siku hiyo. Siku hiyo ilikuwa kama imepigwa laana na kukosa baraka za Mwenyezi Mungu. Watu walikuwa wachache ingawa taarifa zilipelekwa kwa watu wengi. Kwa ujumla haikufana kama ile siku ya ndoa ya dada.

***Itaendelea!***



**Muammar Abu Minyar Al Gaddafi**

Serikali ya Gaddafi ilipinduliwa; alirudi Sirte na kukamatwa na kuuawa na wanamgambo wa NTC.

Akiwa mtu mwenye mgawanyiko mkubwa, Gaddafi alitawala siasa za Libya kwa miongo minne na alikuwa mada ya ibada iliyoenea ya utu. Alipambwa kwa tuzo mbalimbali na kusifiwa kwa msimamo wake wa kupinga ubeberu, kuunga mkono umoja wa Waarabu—na kisha Waafrika—na pia maendeleo makubwa kwa nchi kufuatia ugunduzi wa hifadhi ya mafuta. Kinyume chake, Walibya wengi walipinga vikali mageuzi ya Gaddafi ya kijamii na kiuchumi; alishutumiwa baada ya kifo chake kwa ukiukaji mbalimbali wa haki za binadamu. Alilaaniwa na wengi kama dikteta ambaye utawala wake wa kimabavu ulikiuka haki za binadamu kimfumo na kufadhili ugaidi wa kimataifa katika eneo hilo na nje ya nchi. Urithi wake unaangaliwa kwa maendeleo na ukatili.

## Historia ya Maisha Yake

### Utoto: 1940 hadi 1950

Muammar Mohammed Abu Minyar al-Gaddafi alizaliwa karibu na Qasr Abu Hadi, eneo la mashambani nje ya mji wa Sirte katika majangwa ya Tripolitania, Italia Magharibi mwa Libya. Gaddafi alikuwa mtoto wa pekee kwa wazazi wake na mdogo wa ndugu wanne. Familia yake ilitoka katika kabila dogo lisilo na ushawishi kwa kiasi liitwalo Qadhadhfa, ambao walikuwa Waarabu wa kurithi. Mama yake aliitwa Aisha bin Niran (aliyefariki 1978), na baba yake, Mohammad Abdul Salam bin Hamed bin Mohammad, alijulikana kwa jina la Abu Meniar (aliyefariki 1985); huyu wa mwisho alipata riziki kidogo akiwa mchungaji wa mbuzi na ngamia.

Kama makabila mengine ya wakati ule ya Bedouin ya kuhamahama, familia hiyo haikujua kusoma na kuandika na haikuweka rekodi zozote za kuzaliwa. Waandishi wengi wa wasifu wametumia tarehe 7 Juni; hata hivyo, siku yake ya kuzaliwa haijulikani kwa uhakika na vyanzo vimeiweka mwaka wa 1942 au masika ya 1943, ingawa waandishi wa wasifu wake David Blundy na Andrew Lycett walibainisha kuwa inaweza kuwa kabla ya 1940. Mwana pekee wa wazazi wake aliyesalia, alikuwa na dada wakubwa watatu. Malezi ya Gaddafi katika utamaduni wa Bedouin yaliathiri ladha yake binafsi kwa maisha yake yote; alipendelea kuishi jangwani kuliko mjini na mara nyingi amekuwa akirudi huko ili kutafakari.

Tangu utotoni, Gaddafi alifahamu ushiriki wa wakoloni wa Ulaya nchini Libya; taifa lake lilitawaliwa na Italia, na wakati wa Kampeni ya Afrika Kaskazini ya Vita vya Pili vya Dunia ilishuhudia mzozo kati ya majeshi ya Italia na Uingereza. Kulingana na madai ya baadaye, baba mzazi wa Gaddafi, Abdessalam Bouminyar, aliuawa na Jeshi la Italia wakati wa uvamizi wa Italia wa 1911. Mwishoni mwa Vita Kuu ya Pili ya Dunia mwaka 1945, Libya ilitekwa kwa mabavu na majeshi ya Uingereza na Ufaransa. Uingereza na Ufaransa zilifikiria kuligawa taifa hilo kati ya himaya zao, lakini Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UN) liliamua kwamba nchi hiyo ipewe uhuru wa kisiasa, na mwaka wa 1951 iliunda Uingereza ya Libya, taifa la shirikisho chini ya mamlaka yake. Uongozi wa mfalme anayeegemea Magharibi, Idris, ambaye alipiga marufuku vyama vya kisiasa na kuweka mamlaka katika mikono yake mwenyewe.

***Itaendelea..***

# SAKO KWA BAKO:

## Baadhi ya waliopamba safu yetu 2023

"Wandishi wa vitabu nawambia zipendeni kazi zenu na msiogope wa somaji pale wanapo taka kujua visa vya vitabu vyenu. Wengi wenu hampendi kuulizwa maswali tena mnachukia. Mimi mmojawapo, napenda kuwauliza maswali waandishi, lakini wengi wananichukia kwa kuwaulizauliza."

*Zamira Sanguti*






"...vitabu vimekuwa na mchango mkubwa sana kwenye maisha yangu hasa katika kunisaidia kufanya maamuzi katika mambo mbalimbali, kutoa ushauri na kuelimisha wengine pale inapohitajika na vilevile kunipa burudani..."

*Anna Meleiya Mbise*

"Wito wangu kwa wazazi wa kitanzania naomba tuwajengee watoto utamaduni wa kujisomea vitabu na kupunguza matumizi ya simu na michezo isiyokuwa na ulazima kwani itawajengea tabia ya udadisi pamoja na kuwapa maarifa mapya ambayo yatawasaidia katika maisha yao."

*Martin Mazungwa*





"Maarifa yamefichwa kwenye vitabu, kusoma kunaongeza uwezo wa kufikiri, kuyaelewa mambo, kunatoa exposure (sijapata neno sahihi la Kiswahili), kuuona ulimwengu na maisha nje na mbali na maz-ingira yanayotuzunguka. Vile vile kusoma ni buruda-ni kubwa ya watu wanaopenda utulivu."

*Lulu Siwaya*

**Heri ya Mwaka mpya kwenu nyote...**

# KISASI CHA HISIA— 03

**Ibada ilifanyika kisha safari ya kwenda kuzika ikaanza,ilikuwa ni safari iliyochukua dakika kumi kwa gari hadi kufika makaburini na hapo tulikuta kaburi tayari limeshaandaliwa safari ya kuuweka mwili wa Dayana ikafuata**

***Endelea...***

Baada ya kumaliza kumpumzisha Dayana kulikuwa na wosia ambao Dayana alikuwa ameuacha na kuomba umfikie Lukas lakini iliombwa usomwe mbele ya watu kabla hujafika kwa Lukas

Akaanza kusoma mmoja wa ndugu wa karibu wa Dayana

Anasoma kama ilivyoandikwa...

*"Ngoma ilipopamba moto ndipo muziki ulizimwa ghafla. Kama sio wa leo basi wa kesho ila hali yangu i taabani" Hapo kila mtu aliyehudhuria mazishi yale eneo la makaburi alikuwa kimya kusikiliza ujumbe mujarabu ulioachwa na marehemu siku moja nyuma kabla hajafa. Msomaji akavuta utulivu wa eneo hilo kuangalia kama unatosha kuendelea kuusoma waraka ule.*

Ukimya ulishika hatamu kila mtu alikaa kimya huku wafiwa wakiendelea kububujikwa na machozi bila kukoma

"Naendelea Kusoma kama ulivyoandikwa...."

*Anaandika Dayana*

*Ulikosa nini kwangu, ulikosa kipi mbona nilitenda kila kitu ulichotamani nifanye ili wewe ufurahi.Yani...... Yani niliijali furaha yako hata kama kwangu ilileta huzuni. Mbona niliweka poni huzuni yako na kukukopesha furaha yangu pale nilipoona huna furaha ulitaka nikufanyie nini chenye thamani zaidi ya upendo wangu.*
*Ona ulisababisha nigombane na familia yangu. Nilibadili dini kisa wewe kwa nini...? Kwa nini lakini uliruhusu furaha yangu ipotee kati kati ya bahari ya huzuni, uliyafanya mangapi mbona nilizikuta Sms za*

**<u>Crarens Sanga</u>**



*wanawake wengine kwenye simu yako na bado nikakuomba msamaha mimi. Kipi nilikuwa sijakamilika kukufanyia wewe kipi ulitaka tena kwangu Lukas.*

*Wanaume wangapi walinihitaji ili waje kuwa na mimi lakini niliwakataa wangapi, najua unawajua wote wenye mali zaidi yako na wenye nguvu za kiuchumi kuliko wewe lakini mimi nilikubali kubaki na wewe, mbona sikuyumba kwa namna yoyote ile. Haya ndo malipo yako kwa upendo wangu kweli?*

*Unamkumbuka yule mwanaume Rahim. Najua unamkumbuka ila ngoja nikukumbushe zaidi.....*

*Hakuna upendo wa kweli kama bado hujajua nini maana ya kuumizwa.*

*Naandika haya na Rahim popote alipo anisamehe kama atapata barua hii ningali hai mwite aje nimuombe msamaha na kama atapata hii barua nikiwa kwenye jeneza mwambieni nilikuwa mjinga kati kati ya werevu wake.*

*Rahim mwaka mmoja uliopita alikuja na vipande vya posa pamoja na pete ya uchumba ili aje anioe aliandaa sherehe ili aje anivishe pete. Ndio ni Rahim yule yule mwanajeshi, najua unamkumbuka ni ule upendo wangu kwako nilioutoa kafara juu yako nilikataa pete ya Rahim na kuikubali furaha yako najua nilimsababishia maumivu naomba mkikutana nae niombeeni msamaha leo upendo wake umekuwa fimbo unanisurubu.*

Hapo umakini ukaongezeka na idadi ya watu wenye mioyo myepesi waliungana na wafiwa kuendelea kububujika machozi.

Aliyekuwa anasoma ule wosia alikuwa ameweka kituo kidogo kisha akavuta pumzi ndefu na kuendelea...

*Sikuwa mjinga Lukas, sikuwa mjinga hata kidogo kubadili dini kwa sababu yako. Labda ulijua nilikuwa mjinga lakin kwangu niliona ni zawadi kubwa sana nimeitoa kwako. Nilijitoa muhanga katika kila jambo lililokuhusu wewe, nilikuweka wewe mbele ndio uhai wangu ukafuata kila nilichokifanya kilianza na wewe yote haya hukuyaona*

*Lukas sikutaka niishuhudie harusi yako ndio maana nikaamua niondoke katika*

# KISASI CHA HISIA — 03



*huu ulimwengu ambao ulikuwa unanipa furaha, sioni tena sababu za kuendelea kuivuta pumzi hii hii wanaovuta watu wenye usaliti kama wewe.*

*Ulishindwa nini kuniambia kama hunitaki mpaka ukaamua kutumia njia ya kadi kuzielezea hisia zako kwangu*

*Najua imebaki siku moja tu toka leo naandika waraka huu inafuata ndoa yako. Hongera na ninakutakia maisha mema ndani ya ndoa yako Lukas. Ukipata huu ujumbe jua nimeuandika nikiwa katikati ya uhai na kifo huenda ndio ukawa waraka wangu wa mwisho nauandika katika uhai wangu.*

*Sina mengi ya kukuelezea steve nakutakia ndoa yenye baraka.*

Hapo msoma waraka alimaliza kuusoma huku wengi wa watu waliokuwepo pale miili yao ilishikwa huzuni na ganzi

"Hio ndio ilikuwa siku Lukas anaoa huku Dayana akiwa anazikwa"

Baada ya kumalizika kusomwa kwa wosia ule kila mmoja alitawanyika huku wengine wakizitupa laana za wazi wazi kwa Lukas, lakini Steve kwa wakati wote yeye mawazo yalikuwa kwenye ile namba iliyomtafuta ikidai kuwa inabahasha yake toka kwa marehemu

Steve alidhani huenda ni barua moja iliyosomwa pale makabulini na aliyopewa mtu mwenye ile namba amfikishie yeye.

Saa kumi na mbili jioni ilimkuta Steve akiwa nyumbani kwao huku akiwa na miadi ya kutembelewa na mgeni ambaye hamjui ni nani, ilipotimia saa mbili usiku Steve alipewa maelezo ya kuwa waende kwenye nyumba aliyokuwa akiishi Dayana mara ya kwanza hivyo Steve alijiandaa ili awahi kufika eneo la miadi bila kuchelewa. Saa tatu kamili ilimkuta akiwa tayari kafika eneo la tukio

Alimpigia simu muhusika na kwenda kumchukua kisha waliingia ndani. Chumba kilikuwa kimepangwa vile vile kama alivyokiacha mara ya mwisho anaondoka hisia za kuwa yupo na Dayana zilikuwa zinamzunguka kichwani mwake kuna muda alimuona Dayana akiwa amelala pale Kwenye sofa alilomuacha mara ya mwisho anaondoka lakini alihisi ya kuwa yalikuwa ni mawenge tu hivyo aliachana nayo wakati huo mwenyeji wake alikuwa anamalizia kuandaa chakula cha jioni.

"Umesema unaitwa nani" aliuliza Steve

"Naitwa Enjo sijajua wewe unaitwa nani"

"Naitwa Steve" aliongea kisha akamalizia

"Ulianza urafiki lini na Dayana, na ilikuwaje akafikia kuchukua maamuzi magumu kiasi hiki"

"Ni rafiki yangu wa toka utotoni wewe ndio nikuulize maana ndio kwa mara ya kwanza nakuona toka nifahamiane na Dayana" aliuliza enjo

Hapo Steve alieleza mambo yote toka anapewa kadi na Rachel hadi kufahamiana na Dayana. Ni kipindi wote walikuwa kwenye maumivu ya kumpoteza rafiki yao kipenzi.

JAMVI la SIMULIZI
www.richardmwambe.com

"Taarifa ya kifo cha Dayana ulipata wapi" Steve aliuliza

"Nilipigiwa simu na yeye mwenyewe kuwa hajisikii vizuri, nikaenda nikamchukua na kuanza kumpeleka hospital tukiwa njiani ndio alipoteza maisha tulipompeleka hospital walisema ya kuwa ile sumu aliyokunywa mara ya kwanza iliharibu maini sana hakukuwa na njia nyingine ingekuweka hai hata kama tungemuwahisha hospital" aliongea Enjo

"Na ni bahasha ipi hio aliyokuachia ilikuwa na ujumbe sawa na uliosomwa pale makaburini" Steve akauliza.

Hapo Enjo alitembea hadi kwenye kabati na kuchukua ile bahasha na kumkabithi Steve. Steve aliipokea na kuifungua kisha akaanza kuisoma jinsi ilivyoandikwa.

***Itaendelea***

***Ngoma ilipopamba moto ndipo muziki ulizimwa ghafla***

**"Aaaa kwani hujui kama mi ni Sensei! Nina Dan degree ya juu, sikuipata hivihivi…" Madam S akamwuliza huku akijifuta jasho usoni na kumpita mwanadada huyo huku akielekea kwenye vyumba maalum vya kubadilisha nguo.**

"Kabisa, unastahili cheo hicho…" Gina akamwambia Madam S kisha akawageukia Amata na Jasmine, "Wawili wote mmepigwa, lo! Serikali imekula hasara…" Gina akaendeleza utani kwa Amata aliyekuwa naye akitoka kuelekea upande mwingine wa jengo hilo kubwa. Mara ukasikika mlio wa kitu kama kengele uliolia mara moja tu na haukujirudia. Ishara hiyo ilijulikana kwa wote kuwa dakika kumi zijazo wote walitakiwa kukutana katika ukumbi wa mikutano, ikawa hivyo.

*** *** ***

Madam S alikutana na vijana wake katika ukumbi huo mdogo ambao ulitumika zaidi kwa mazungumzo ya hapa na pale huku chupa ya maziwa ikiendelea kupita.
"Mmepata habari kutoka Kenya?" akawauliza.
"Zipi tena?"
"Matajiri wakubwa wawili wameuawa ndani ya saa nane tu, mmoja kauawa Nairobi na mwingine Kinangop," Madam aliwaeleza.
"Hiyo hata mi sijaisikia…" Kamanda alidakiza kusema.
"Ah! ndiyo hivyo," akaendelea huku kikombe kilichojaa maziwa kikienda kinywani.


"Sasa wanamdhania nani?" Chiba akawahi kuuliza.
"Ah! Sijafuatilia si unajua huu udaku tu," akaendelea.
"Wamekufaje kabla ya kujua wa kumdhania," Amata akataka kujua.

"Tatizo lenu hamsomi mitandao, hizi habari mbona zipo mitandaoni tangu alfajiri? Huyo aliyeuawa Nairobi alikuwa na mwanamke ndani inasemekana kadunguliwa na huyo wa Kinangop sijui sumu sijui, haieleweki," Madam S akaendelea kuwaeleza.

"Lakini mbona hata hapa matajiri wanauawa tu, si visasi na kudhulumiana, isitoshe vifo vinaweza kuwa havina uhusiano nikiwa na maana kuwa kila mmoja kafa na lwake," Gina akachangia.
"Ya Ngoswe mwachie Ngoswe mwenyewe, leteni ripoti. Swala hili nataka sote tuliweke sawa. Lete ripoti Chiba," Madam akawakatisha.

"Baba Askofu ameondoka kuelekea London," akajibu kwa mkato. "Kama nilivyokwambieni, huyu Askofu hata kama ni kiongozi wa dini lazima achunguzwe kwa kina kwa sababu kuna vitu ambavyo naona kama haviendi sawa. Yupo yeye na yule mwingine sijui nabii nani sijui huyohuyo!" Madam S akaeleza.

"Wakati tunarudi tumekoswakoswa ajali pale Vingunguti," maneno hayo ya Gina yakawafanya wote kuweka vikombe mezani.
"Ajali?!" akauliza Jasmine.
"Ndiyo na gani namba T 45f JKL, Land Rover County" akaeleza.
Madam S alitulia kimya wakati akiisikiliza habari hiyo huku ubongo wake ukifanya hesabu kuwa moja na moja ni kumi na moja ila moja jumlisha moja ndiyo mbili.
"Vipi Madam?" Gina akauliza.
"Naifikiria hiyo ajali… sina uhakika kama ni ajali sana au la…" akaeleza.




"Na hilo gari tumelikuta hapo karibu kabisa na Daraja la Kigamboni limeegeshwa lakini ndani yake hamna mtu," Gina akeleza.
"Ok! T 45f JKL, lipekueni haraka tuone kama kuna lolote," akaagiza na Chiba akanyanyuka na kuingia kwenye kijichumba fulani hivi.
Pale mezani kila kitu kilikuwa kikiendelea kama kawaida na mara hiyo simu ya Madam ikaita kwa fujo. Akainyakuwa na kutazama namba ya mpigaji. Scoba!

"Niambie mwanangu…"
"…Windo limeondoka, kama nusu saa hivi na nimelifuatilia nimeona linaelekea Uwanja wa ndege…"
"Copy and clear, rudisha mkia bandani," akamjibu kisha akakata ile simu na kuinuka. "Narudi," akawaambia. Kikao kile hakikuchukua muda mrefu, kila mmoja alitawanyika na kuendelea na jukumu lake.
Akiwa ndani ya ofisi yake ndogo, peke yake, bila bugudha aliketi na kuyavuta mafaili yake mawili na kuyasogeza karibu, kisha akaichukua miwani yake na kuipachika usoni tayari kwa kupitia hili an lile.

Kabrasha la kwanza lilikuwa limeandikwa 'Bishop Bariki Zebetoni', na ndani yake kulikuwa na nyaraka kadhaa zikiwemo za utajiri wake na safari zake zote wapi anakwenda na kufanya nini. Madam S alikuwa akihifadhi kumbukumbu hizo tangu alipoanza kuwa na shaka naye.

Na la pili liliandikwa '*Nabii Ezekiel Bayankata',* nalo kama lile la kwanza lilikuwa na makabrasha kadhaa yaliyoeleza utajiri wa kupindukia wa Mtu wa Mungu huyo anayejiita 'nabii', huku nyuma yake sijui hata huwa anafanya nini. Hakukuwa na wa kumuuliza, jaribu; ufukuzwe kwenye ushirika? Isitoshe misaada iliyokuwa ikitolewa na nabii huyo nani mwingine angeweza? Hata pale ambapo serikali ilishindwa kufika kwa namna moja au nyingine yeye alifikisha msaada au huduma iliyokuwa ikihitajika.

Na upande wa Askofu Bariki ulikuwa hivyo; shule, hosiptali na misaada mingi tu alikuwa akiwapatia wananchi. Nje waumini walifurahi na kuusifu upendo wa viongozi hao kwa Kondoo wa Bwana, lakini wahenga walisema 'Siri ya kaburi aijuaye maiti'. Kilichomshangaza Madam S ni ukaribu wa watu hao wawili ulioibuka ghafla kiasi kwamba watu waliutilia shaka. Imeonekana mara kadhaa askofu huyu akikutana kwa siri katika hoteli fulanifulani na nabii huyu. Nini walikuwa wanazungumza? Hakuna aliyejua, lakini wadukuzi wa mambo walizivujisha habari hizi na ndipo watu wa usalama walipoamua kulivalia njuga suala hili kuchunguza utajiri na uhusiano kati ya watu hao wawili.

Baada ya uchunguzi wa awali ndipo ilipogundulika kuwa utajiri wa bwana huyo hautokani na kazi za kanisa wala wafadhili wake, na hapo ndipo utata ulipoanza na uchunguzi wa chini kwa chini ukachukua nafasi.

"London … Kuna nini?" Madam akajiuliza kwa sauti huku akigongagonga kalamu yake mezani. Nukta hiyo hiyo, simu yake ikapata uhai, akainyakuwa na kuiweka sikioni.
"Ndiyo kijana (…) njoo mara moja ofisini kwangu…!" akamwambia huyo aliyepiga simu hiyo.
Punde si punde, Scoba aliungana na Madam S ndani ya ofisi hiyo.
"Amesafiri kama ulivyodhani," akamwambia Madam S.
"Enhe… ameenda wapi?
"London, nimejaribu kuongea na waumini wake pale katika kanisa lake nikijifanya nahitaji huduma ya kiroho kutoka kwa nabii huyo lakini nikaambiwa nirudi baada ya siku tatu au nne…"

"Ndiyo atakuwa amerudi?"
"Ndiyo," Scoba akajibu.
"Good! Sasa naelewa elewa kidogo lakini una kazi zaidi ya kufanya. Endelea kuwa muumini wa kanisa hilo na hata hiyo kesho kutwa unayotakiwa kwenda hakikisha unaonana naye…"
"Sasa nikionana naye nitamwambia nini?" Scoba akamkatisha Madam S sentensi yake.
"We nenda, ya kumwambia Roho Mtakatifu atakupa hukohuko." Kauli hii ya Madam S ilimfanya Scoba kuangua kicheko na kutoka ndani ya ofisi ile.

**SURA YA 04**

MAJIRA ya saa tisa alasiri kwa saa za Uingereza, mjumbe wa mwisho wa kundi la Cron aliwasili kwa ndege ya shirika la Lufthansa akitokea Germany. Moja kwa moja alielekea katika mji mdogo wa Cunglia, huko mashambani. Huko alikutana na wengine ndani ya nyumba moja iliyojitenga kabisa na nyingine. Cha kushangaza nyumba hiyo ilikuwa katikati ya uwanja mkubwa wa makaburi ya zamani.

Chumba kilikuwa na mwanga mzito mwekundu na wote walikuwa ndani humo walivalia mavazi mekundu na kufanya kwa namna moja au nyingine kutoelewana vyema sura zao, na hii ilizidishwa na kuta za chumba hicho, maana nazo zilikuwa na vioo vilivyozidisha rangi hiyo.

Aliyekuwa kama kiongozi kati yao aliinua uso wake na kutazama jopo lililofika la wajumbe saba.

***Itaendelea...***

**Kitabu cha CRONOC 7—chapa ya pili kitakuwa madukani mwezi wa Februari, 2024.**

**Weka oda yako sasa kwa kutuandikia whatsapp 0766974865.**

**Na ukipenda kulipia kabisa waweza fanya hivyo kwa kutuma pesa '12,000/=' kwenda Mpesa Lipa Namba 5559006 JAMVI LA SIMULIZI kisha tutumie meseji ya muamala wako kwa whatsapp hiyo hapo juu.**

"Sasa ni wakati wa kuondoka", alijisemea Kassim. "sitaki kukaa hapa muda mrefu mwishowe wale wezi wanikute humu watakaporudi! Nimeshapata mali nyingi sana ya kutosha kujaza masanduku yote kumi yaliyobebwa na punda wangu. Nitarudi kesho na siku inayofuata na inayofuata hivyohivyo mpaka mali yote hii niimalize, lakini kwa leo inatosha wacha tu nirudi nyumbani"

Kwahiyo basi, Kassim akaanza kusema yale maneno ya siri yakufungulia pango lile ili atoke nje. "Fungukaaaaa ……….!!!" Lakini alisahau neno linalofuata! Alijaribu tena, "Fungukaaaa…..uummh!!!" , loh! masikini Kassim kasahau kabisa neno linalofuata. Akajaribu kwa mara nyingine tena. "Fungukaaaa…eeee ssssiiisss!!!, hapana sio hivyo, ah nimeshasahau neno lile! Mlango uliendelea kuwa umefunga kwa kuwa neno lile Kassim hakuweza kulikumbuka ambalo ndio la kufungulia lango lile. Kassim akaanza kutetemeka kwa hofu. Akaanza kuvuja jasho. Alikuwa na hazina nyingi pale kashazikusanya lakini hazitasaidia kitu chochote endapo mlango utashindwa kufunguka.

"Muda wote nilikuwa nafikiria mali tu na kusahau neno la siri!", alilia Kassim. Alijilaumu sana. " Sasa nimekamatika leo" alisema Kassim. Alitupa begi la dhahabu alillokuwa amelibeba na kulipiga teke kama mpira wa miguu. "nilifikiri nitakuwa tajiri sana, kumbe ni marehemu mtarajiwa" Alijiwazia Kassim.

Mara Kassim akasikia sauti ambayo ilibadilisha damu yake kuwa barafu. Alisikia sauti za kwato za farasi zikija kwa vishindo kutoka mbali kidogo. Walikuwa ni farasi wapatao arobaini (40) na walikuwa wameshakaribia kufika kwenye mlango wa pango lile.

"Fanyeni haraka! Tuziweke hizi hazina ili tuondoke haraka tukatafute tajiri mwingine wa kumuibia!" Kiongozi wao alisema. Na huku wenzake wakiwa wakicheka. Walikuwa wanakuja kuweka mali pangoni ambazo wametoka kuziiba.

Lakini walipokaribia kufika katika jiwe kubwa la pango, kiongozi wao akaona kitu ambacho kilimkasirisha sana. Kulikuwa na punda kumi waliokuwa wamesimama nje ya pango lile wakiwa na masanduku makubwa juu ya migongo yao.

"Kuna mtu anajaribu kutuibia mali zetu!!", kiongozi wao alisema. "Lazima tumkomeshe mara moja!!". Wale wezi walipiga makelele ya hasira huku wakipiga makofi, punda wote kumi walishikwa na hofu na kukimbilia msituni. Kwa taratibu kabisa wezi wote walishikilia panga zao kali huku wakikaribia lango la pango lile.

"Fungukaaaaa sesmiii!!!", alisema Kiongozi wao. Lango kubwa la jiwe likaanza kufunguka. Ghafla Kassim alitoka mbio nje kulekea kwa kiongozi wa wale wezi huku akipiga makelele na kumkamata na kuanza kupigana. Alijitahidi sana kupigana ili aweze kuokoa maisha yake, lakini mmoja kati ya wale wezi alimchoma panga tumboni na hatimaye Kassim akaanguka na kufa palepale.

Wezi wale arobaini walimuacha Kassim chini na kuingia pangoni, "angalia hii mifuko ya dhahabu hapa mlangoni!!" alisema mmoja wa wale wezi, "huyu alikuwa amepanga kuzichukua hizi zote na kuzipeleka kwa wale punda wake kumi!".

"Alikuwa peke yake huyu?" Aliuliza kiongozi wao. "kwasababu baadhi ya dhahabu zipo hapa mlangoni na zingine hazipo kabisa humu pangoni!, huenda ni zaidi ya mtu mmoja alikuwepo humu pangoni wakiiba hazina zetu! kwahiyo watu wawili wamegundua neon letu la siri la kufunguli apango hili!!"

"Sasa sijui tufanye nini" alisema mmoja wa wale wezi.

"Tumemuua mmoja!" Alisema kiongozi wao. " Na huyu mwingine tutamtisha kwa njia moja ama nyingine, hatathubutu tena kutuibia chochote hapa!!". Alinyanyua upanga wake juu hewani huku akitoka nje ya pango.

***ITAENDELEA!***



# SAFARI YA SAN FRANSISCO

## Ameandika Fadhy Mtanga

MWAKA 1999 nilikuwa mwanafunzi wa kidato cha tatu wa Shule ya Sekondari Njombe. Miongoni mwa vitu nilivyokuwa navyo, ni daftari kadhaa ya nyimbo za reggae, R&B na Hip Hop. Kwenye moja ya daftari hizo, mimi na rafiki zangu tuliweka taarifa tulizoziita autobiography. Kwenye ukurasa wangu, sehemu ya Best City niliandika majiji mawili: Kingston, Jamaica na jiji jingine, San Francisco, Marekani

Sasa ni miaka 24 tangu nilipoandika vile. Na leo hii, ninaandika hapa nikiwa orofa ya 5 ya hoteli ya Kimpton Alton, jijini San Francisco ndani ya jimbo la California hapa Marekani. Na wakati huu ikikaribia saa nne unusu ya asubuhi, ninafahamu ni saa tatu unusu nyumbani Tanzania. Kabla hujalala, nimeona nikuandikie kidogo. Na, nitaandika harakaharaka kwa kuwa ifikapo saa 5 nitaanza safari ya kupita kwenye handaki la chini ya bahari ya Pasifiki ili kuzuru jiji la Auckland.

Wakati nikikuandikia, tayari nimeshapita juu na chini ya Golden Gate Bridge kwa kutumia basi na boti mtawalia. Tayari nimeshapanda ngazi 234 kwenye orofa 13 za Mnara wa Coit. Nimeshatembelea Gereza la Alcatraz, gereza maarufu mno kama 'Mwamba', tayari nimekwishatembelea mitaa yote ya San Francisco kwa basi maalumu. Nimekwisha panda milima na kushuka mitaa yote adhimu. Nimekwishakula chakula cha Kimeksiko, tacos; ya samaki, ya ng'ombe na ya kuku. Nimekwishakunywa miongoni mwa cappuccino bora zaidi ulimwenguni. Nimekwishazuru majengo marefu na ya kihistoria kama kiwanda cha chokoleti cha Ghirardelli. Na zaidi, nimetembelea duka kubwa na kongwe la vitabu na uchapishaji la City Light.

Kwa nini nipo San Francisco. Mwezi Novemba 2021 niliandika hadithi fupi: Haiba. Na nikikusimulia kilichonisukuma kuandika, utacheka. Waswahili husema, heri huzaliwa katika tumbo la shari. Siku chache baada ya kuposti simulizi hiyo mtandaoni, mtu mmoja aliniandikia kupitia kibobo cha Twitter *(nasikia siku hizi mnaita X)* kuomba idhini yangu kuitafsiri kwenda Kiingereza. Sikuona shida. Nilimruhusu. Mwezi mmoja baadaye, nikaandikiwa barua-pepe ya kuombwa akaunti yangu ili kulipwa kutokana na simulizi hiyo. Na kwa kuwa wakati huo nilikuwa njiani kuelekea mapumziko ya Krismasi na Mwaka Mpya, nikasema, *'aaah, mambo si ndo haya!'*

Miezi michache baadaye, nikaombwa idhini ya simulizi hiyo kutumika kwenye mkusanyiko wao wa kwanza wa simulizi kutoka Afrika Mashariki. Kwa hakika, nilikubali nikiwa na furaha tele. Kwangu, ilikuwa hatua adhimu mno katika uandishi wangu. Na wakati haya yakitokea, nilikuwa nimekwishafikiria kustaafu kuandika kutokana na sababu kadha wa kadha.

Siku moja mwishoni mwa mwezi Mei mwaka huu, nilipokea barua pepe kwenye akaunti binafsi. Kwa kuwa kichwa kilianza na '*Invitation to…*' nilitaka kuipuuza nikiamini ni zile barua pepe za kawaida zinazokuja mara nyingi. Kitu kikaniambia niifungue. Na nilipoona ni mwaliko wa kuja Marekani kuhudhuria maadhimisho ya miaka 10 ya kampuni mufti ya uchapishaji wa vitabu hapa Marekani, nikasema, '*eeh b'ana eeh!"* Nilipojibu kukubali, nikapokea maelekezo yote na taratibu za kuomba viza zikafanyika kwa mafanikio. Na barua ya mwaliko ikanitaka kuja kusoma simulizi ya Haiba (ambayo inafahamika kama Attitudes kwenye kitabu cha mkusanyiko wa riwaya kutoka Afrika Mashariki, No Edges). Na jambo la kuvutia, mfasiri wangu, Jay Boss Rubin alialikwa pia. Naye, alisoma tafsiri ya Kiingereza.

Jana, kumefanyika maadhimisho hayo hapa San Francisco. Na kwa heshima kubwa, nilipewa nafasi ya kusoma kipande cha simulizi hiyo mbele ya wachapishaji na waandishi wakubwa. Fikiria, unasoma simulizi mbele ya mwandishi bingwa wa Kimeksiko, Jazmina Barrera, ama mfasiri nguli wa Kichina, Jeremy Tiang, ama mbele ya mhariri bingwa Kesley McFaul. Na baada ya kusoma, kwenye hafla ya usiku, nikaimba wimbo maarufu zaidi wa Kiswahili, Malaika.

Wakati nataka kumalizia kwa leo, niseme hivi: Ushirikiano wangu na kampuni hii, ambayo pia imefanya kazi na mwandishi mwenzangu …

***…Inaendelea ukurasa wa 07***

# SHUBAKA LA VITABU

**Katika Safu yetu ya SHUBAKA LA VITABU leo tutawaletea Maktaba kumi (10) bora duniani. Je; wazijua hizo. Karibu uwe nasi upate kujua haya,**

**5. MAKTABA YA TAIFA YA CANADA**
(Maktaba na sehemu ya kutunza kumbukumbu)

Hii ni maktaba ya tano (5) kwa ukubwa duniani. Mara ya kwanza ilipoanzishwa mwaka 1872 ilikuwa Maktaba na sehemu ya kuhifadhi kumbukumbu 'LAC'.

Halafu mwaka 1953 ikafanywa kuwa maktaba mwaka. Mwaka 1912 iliitwa Kituo cha Kutyunza kumbukumbu cha Canada. Mwaka 2004 kituo hicho na maktaba vikaunganishwa na kuwa kitu kimoja.

Maktaba hii inapatikana Mtaa wa Wellington katika jiji la Ottawa. Ndani yake imehifadhi nyaraka nyingi mno, kama vile; Magazeti, michoro ya majengo, mabaki ya vitu anuai vilivyobeba historia, maandiko ya kifasihi ya watoto wa Canada, vitabu vya vibonzo vya Ki-Canada, machapisho ya kielektroniki, filamu bunilizi na zisizo bunilizi, machapisho ya kiserikali nk.



Inakadiriwa kuwa na vitabu Milioni 22 na machapisho ya serikali, michoro na ramani za majengo Milioni 3, picha Milioni 30, filamu zenye urefu wa saa 350,000 na picha za kisanii 425,000. Aidha kuna miziki 547,000 na kazi za kidijitali zenye ukubwa wa Mega Bite bilioni 1.

Maktaba hii ina wafanyakazi 853 na bajeti yake ni Dolari za Ki-Canada 98, 346, 695 kufikia mwaka 2014.

**6. MAKTABA YA DOLA LA URUSI**
Maktaba hii usiichanganye na ile Maktaba ya Taifa ya Urusi. Hizi ni mbili tofauti. Na hapa tunazungumzia *Russia State Library*. Maktaba hii ilianzishwa tarehe 1 Julai mwaka 1862. inapatikana jijini Moscow na ni sehemu ya makumbusho ya Umma ya Moscow na Makumbusho ya Rumyantsev.

Katika maktaba hii kuna makusanyo milioni 47.7 ikiwamo vitabu, majarida, magazeti, sauti na rekodi za muziki, ramani, mihuri, michoro na miswada mbalimbali.

Ina wafanyakazi 1,699 na wanachama 387,000. bajeti yake inakadiriwa kuwa ni fedha za Kirusia bilioni 2.4.



*ITAENDELEA*

***Makala imeandaliwa na R. Mwambe***

# KITABU NILICHOSOMA

**Anna Mbise Mobile Library**
**JINa LA KITABU: Mikono iliyo-barikiwa (Gifted Hands)**
**JINA LA MWANDISHI: Ben Carson**
**JINA LA MSOMAJI: Isack Akyoo**
**TOKA: Zanzibar**

NILIYOJIFUNZA KWENYE HIKI KITABU

1. Nafasi ya Wazazi katika kuchangia Mafanikio ya watoto hapa Duniani, Mfano Sonya anavyo watia moyo Ben na Curtis katika masomo yao.

2.Changamoto siyo mwisho wa maisha bali ni chachu ya mafanikio, Sonya Carson mama yake Ben Carson anaibuka shujaa baada ya kujibidiisha kufanya kazi kwa bidii pamoja na kuwa hana elimu ya darasani lakini ana Elimu ya maisha hivyo hachagui kazi kitu kilichopelekea watoto wake kufanikiwa kwa kusimama nao bila baba baada ya ndoa kuvunjika.

3.Ndoa za ututoni zinaathiri jamii hata sasa kwa kua watoto chini ya miaka 18 na kupeleka kuua NDOTO ZAO, KIPAJI NA MAFANIKIO YAKE YA BAADAYE, Mfano Sonya Carson aliolewa akiwa na miaka 13 .

4.Ndoa za mitala zina changamoto kama kuzalisha matatizo kwenye jamii kama hii ya Carson, Sonya na Mke mkubwa ilivyopelekea upweke kwa watoto wao na kupitia shida ambazo zilikuwa ziepukike kwa kuacha tamaa. Kwasababu hata huku mitaani kuna wanaume wanakuwa na wake zaidi ya mmoja nje ya uwezo wao Kibayolojia, Kiuchumi na Kiutawala.

5.Mtangulize Mungu katika kila jambo unalofanya nawe utafanikiwa,hapa tunakumbushwa na Ben pale alipokuwa amejitahidi kuacha tabia za hasira lakini alipomshirikisha Mungu aliweza.

6.Somo jingine hapa Mimi ni Nahodha wa maisha yangu hivyo napaswa kujisimamia ili kuepuka aibu katika maisha, hapa namuona Sonya Carson akinukuu mstari shairi la Mayme White Miller "Wewe ndiye nahodha ya meli yako"
Hivyo ukianguka ujilaumu mwenyewe.

7.Kujichunguza pale mambo yanapokwenda mrama, wakati mwingine tunaharibu mahusiano wenyewe na kubakia kulaumu wengine wasiohusika. Hivyo Sonya anatukumbusha kujichunguza panapotokea sintofahamu usikimbilie kulaumu wengine.

8.Kuwekeza kwenye Afya kama Taifa ili panapo tokea changamoto za Kiafya inakua rahisi kutatua kama ambavyo ilitokea kwa Mapacha na kina Timu Johns Hopkins walivyotoa Ushirikiano.

9.Tuwasaidie watoto wetu kufikia NDOTO zao ili wakaisaidie jamii katika viwango vikubwa kama ilivyotokea kwa Ben kuwa na Ndoto ya kuwa Daktari na baadaye kuanzisha Taasisi ya kuwasaidia vijana wenye Talanta zao kufikia NDOTO zao pale wanapokuwa wamekwama kutokana na uchumi mdogo wa familia.

10.Tuisaidie Jamii yetu kwenye changamoto tunazoziweza

11.Upendo na Umoja ni nguzo muhimu sana katika familia masikini ili kuinuka kiuchumi kwa kuungana Wazazi na watoto kuwa wamoja na kuweka Malengo ya mwaka na kumtanguliza Mungu mbele utafanikiwa, rejea kwa Ben akinukuu Warumi 8:28


12.Kuna wakati wa kusimama peke yako katika maisha, hivyo utatakiwa kujisimamia, kujiendesha na kupambania unachokiamini kama Ben.

13.Hekima ni muhimu katika familia ili kutunza AMANI, Mfano Ben alitaka kumshambulia Mama yake lakini Kaka yake Curtis alimzuia na kumshauri na hivyo presha ya hasira ikapoa hivyo na sisi tusikubali kufanya maamuzi tukiwa na hasira ili kuepuka LAANA toka kwa wazazi na wazee.

14.Nimejifunza kuukomboa wakati kupitia Sonya, Ben na Curtis

15.Kuwa mtu mwema kwa kutendea watu mambo mema Mungu atakubariki kama ambavyo mafanikio ya Ben yamechangiwa na watu ambao wengine hawana ukoo naye.

16.Nguvu ya malezi ya mama katika jamii.



# MATANGAZO




**TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.**
**Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.**
**Wailiana nasi kwa simu (call & Whatsapp) 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com**

## NAKUPENDA TANZANIA

Nchi yangu Tanzania, nishani nakutunuku
Sana nakufurahia, kwako sina dukuduku
Wewe ninajivunia, nipo nawe kila siku
Nakupenda Tanzania, daima nitakuenzi

Moja tisa sita moja, safari uliianza
Sita nne kwa pamoja, muungano ulianza
Nazipata nyingi hoja, mengi kwako najifunza
Nakupenda Tanzania, daima nitakuenzi

Umejaliwa amani, dunia yakutambua
Mlima wenye thamani, sisi sote twaujua
Unapendwa na jirani, atamani kubekua
Nakupenda Tanzania, daima nitakuenzi

Nimekuchora moyoni, kwako najimwayamwaya
Utosini unyayoni, mambo moto mambo faya
Ukwasi kwako pomoni, kama mkuu wa kaya
Nakupenda Tanzania, daima nitakuenzi

Maji chumvi unyayoni, gotini na sikioni
Yatusafishe machoni, yasiishie sokoni
Tufaidi maishani, furaha iwe moyoni
Nakupenda Tanzania, daima nitakuenzi

Safari tuianzie, ukingoni mwa Kusini
Acha nikusimulie, ufurahi safarini
Mapema uyang’amue, yalofichika sirini
Nakupenda Tanzania, daima nitakuezi

Zao kuu ni korosho, ufuta pia mbaazi
Hata ndizi za Kibosho, zinaatwa na jahazi
Zawadi ya ukum busho, watakupa na viazi
Nakupenda Tanzania, daima nitakuenzi

Upenuni baharini, samaki wapatikana
Msosi ni mkekani, kula kwa kutazamana
Mafunzo ya unyagoni, katu utani hawana
Nakupenda Tanzania, daima nitakuenzi

Tusogee na Rufiji, maji tumetunukiwa
Ardhi ya vile vijiji, rutuba imejaliwa
Wana mengi mahitaji, wasije kusahauliwa
Nakupenda Tanzania, daima nitakuenzi

Nyanda za juu kusini, chakula cha uhakika
Tukijaze maghalani, tusije kuhangaika
Kazi kubwa mashambani,  hili linafahamika
Nakupenda Tanzania, daima nitakuenzi

Kitovu cha biashara, namaanisha jijini
Kule kuna barabara, kila kona ni mjini
Mwendo wataka busara, kujitoa matatani
Nakupenda Tanzania, daima nitakuenzi

Pale makao makuu, zao kuu ni zabibu
Zilipo ofisi kuu, nyumba ya utaratibu
Tambalale siyo juu,  hufiki kwa melikebu
Nakupenda Tanzania, daima nitakuenzi

Tuvuke maji tuvuke,  kisiwa cha karafuu
Zanzibari Chakechake, sogea hadi tunguu
Mambo safi mwake mwake, utarii uko juu
Nakupenda Tanzania, daima nitakuezi

Beti bado zanijia, hapa naweza komea
Sana nimekusifia, vizuri kukusemea
Kalamu naiachia, isije kunigomea
Nalupenda Tanzania, daima nitakuenzi

**Mwl. Elisha Panyenje**
**Malenga wa zama hizi**
**Mbelei—Bumbuli—Tanga**

**elishapanyenje@gmail.com**


**0716249523 / 0622010040**
**Mitandao ya kijamii ELISHA PANYENJE**

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**

# Habari Picha



Siku nilipotembelea Mlimani FM. Richard Mwambe kushoto na DJ Sharif Pinda kulia, tukiwa katika pozi baada ya kukamilisha mwanzo wa makala makini ya kifasihi.



Tunampongeza Ibrahim Gama, kwa kumbukumbu ya kuzaliwa kwake 31/12. Ibrahim Gama ni mmoja kati ya waandishi nguli nchini... ameandika BARUA KUTOKA JELA, KANTANGAZE, BALAA na vinginevyo.



Wanachama watiifu wa Marmz Group walipoenda kutembelea wafungwa katika Gereza la Ukonga tar. 30/12/2023. Hii ilikuwa ni moja ya matukio yao ya kufunga mwaka kwa wanakundi hawa. Mara nyingine wamewahi kufanya hivi katika maeneo mbalimbali yanayohitaji msaaa. Hongereni sana na Mungu awape zaidi.

**Ukilipata jarida hili, mtumie na mwezako.**

**"Tuambukizane furaha kwakuwa siyo ugonjwa"**
**by Luvanda Vitenge**

# KUTOKA MAKTABA: MIAKA 62 YA UHURU—02

**'VITUKO VYA UHURU' - Harakati za kupigania Uhuru wa Tanganyika na vituko vyake. Ni kitabu kilichoandikwa na M.W. Kanyama Chiume—1973**

Ni Hindu Mandal tu iliyodiriki kutoa msaada wa hali na mali kama vile viti ama ukumbi wa kufanyia mikutano ya mwaka ya TANU. Kuwako kwa chama cha kikabila (kinachosemekana kwamba kilikuwa na nguvu sana na fedha nyingi) cha *Uzaramo Union,* kuliwafanya watu wengi hapo awali waidhanie pia TANU kama chama cha kikabila.

Mkoloni pia aliizidisha chuki na tofauti za kidini kiasi kwamba mwaka 1955, TANU ililazimika kuanzisha kikundi cha *Bantu Group* kupambana na tatizo hilo. Mkutano mkubwa uliohudhuriwa na masheikk Hassan bin Amir, Mwinyimadi Ali, Nurudin (Kutoka Lindi) na Chaurembo uliitishwa, na wote walitaka kulikuza balaa hili walilaaniwa hadharani kwa kuambiwa wazi kwamba kila dini duniani ililaani tabia ya mwanadamu kutaka kumkandamiza mwanadamu mwenzake.

Ingawa kutokana na mkutano huo mzizi wa kidini ulitikiswa vya kutosha, lakini wakoloni hawakuacha kuitumia dini ili kuipinga TANU mjini Dar es salaam. Waliwashawishi Waafrika wachache kuanzisha chama cha AMNUT. Hali kadhalika, mkoloni hakuchelea kutumia kuzuka kwa vita vya Mau Mau nchini Kenya kuwaogofya wananchi kutojiunga na TANU kwa vile eti chama hicho kingeanzisha Mau Mau nchini Tanganyika pia!

Njama hizo, kama zote zilizotangulia ama zile zilizofuata, kama vile kuanzishwa kwa vyama vya U.T.P na Congress, hazikufaulu. Jinsi TANU ilivyopigwa vita ndivyo nayo ilivyozidi kuungwa mkono na wananchi. Na baada ya John Hatch, mjumbe wa chama cha Labour Uingereza kuhutubia umati mkubwa wa watu Mnazi Mmoja mwaka 1957, kuyaunga mkono maneno ya Mwalimu Nyerere kwamba Watanganyika walikuwa na haki ya kudai uhuru wao, fukuto la uhuru liliuzingira mji. Maelfu kwa maelfu ya watu walijiunga na TANU.

Kiwango cha mapambano kilikuwa kikubwa kiasi kwamba uvumi mkubwa ulienea Dar es salaam kwamba kwenye mkutano mkubwa wa kihistoria uliofanywa kiwanja cha ndege cha zamani (mara tu baada ya mkutano mkuu wa Tabora juu ya Kura Tatu) mkoloni alitega mabomu ambayo yangelipuka kutokana na joto la sigara. Vijana wa TANU walikesha kukilinda kiwanja hicho kabla ya mkutano.

Na nguvu ya wananchi dhidi ya mkoloni ilionekana mara tu baada ya kesi ya Ndugu Rashidi M. Kawawa, Katibu Mkuu wa T.F.L aliyeshtakiwa, eti kwa kuwatisha wafanyakazi wa E.A Breweries kwa kutojiunga na wenzao katika mgomo (ulioungwa mkono na TANU) dhidi ya kunywa pombe za kizungu. Mara tu baada ya kesi hiyo, umati mkubwa ulimbeba ndugu Kawawa juu kwa juu mabegani kwa vifijo na vigelegele kumrudisha ofisini kwake. Baada ya mkoloni kuadhirika mno, aliutawanya umati huo ukiwa njiani kuelekea Makao Makuu ya TANU, kwa mabomu ya machozi. Japo watu walitawanyika, mabomu hayo hayakutawanya mioyo ya kizalendo. Hivyo ndivyo wananchi walivyouonesha uzalendo wao wakati Mwalimu aliposhtakiwa mahakamani eti kwa kuwakashifu maD.C wa Geita na Musoma. U,ati mkubwa zaidi wa wananchi ulijaa mahakamani kila siku ya kesi hadi alipotozwa faini ya shilingi 3000/- (fedha nyingi sana wakati huo).

Wananchi walizichanga papo hapo na kumlipa mkoloni faini hiyo. Ilipofika 1961 baada ya kila njama za kisiasa na kinyama kushindwa, mji wa Dar es salaam ulisisimuliwa kwa vifijo, gombesugu, zumari na magoma mengine ya kila aina, kwenye maandamano makubwa yaliyoongozwa na lendrova alilokuwemo Mwalimu Julius K. Nyerere akiwa amebeba karatasi kubwa lililokuwa na maandishi—UHURU ESEMBA 9, 1961.

***Uhuru ni lulu kwa wote lakini ni dhahabu kwa wasiokuwa nao.***

***Katika toleo lijalo tutaendelea na Sura ya Pili ya simulizi vii 'VITUKO VYA UHURU"***

# ELIMU KWA WAZAZI NA WALEZI

## HAKUNA MWANAFUNZI ANAYEPENDA KUFELI

Makala haya ni maalum kabisa kwa wazazi na walezi wote wenye wanafunzi mwaka 2024

Moja ya vitu ninavyoviamini ni kuwa hakuna mwanafunzi anayependa kufeli,hakuna mwanafunzi anayetamani kumaliza shule na kukosa cheti. Kufeli ni matokeo ya changamoto nyingi anazokutana nazo mwanafunzi katika safari yake ya kufuta ujinga. Ambatana nami katika kuangalia changamoto hizo kwa uchache wake;

***1: Usimamizi hafifu,*** shuleni kuna wanafunzi wachache sana ambao wanahitaji usimamizi mdogo,walio wengi wanahitaji usimamizi wa karibu sana, mzazi ukimsahau mwanao hata siku mbili jua kuwa umepoteza pakubwa saana. Ikitokea mzazi katingwa,mwalimu naye kazidiwa na majukumu,kwa pamoja wameshindwa kabisa kumsimamia mwanafunzi tambua kuwa mwanafunzi husika hawezi kufanya vizuri kamwe. Mzazi jukumu lake ni dogo lakini linamchango mkubwa sana kwa mwanafunzi. Mzazi inakupasa kutumia dakika kumi ama kumi na tano kumsikiliza mwanao yale aliyojifunza siku hiyo,kumsisitiza kusoma na kuonesha kuwa unamfuatilia. hii ikifanyika kwa mwendelezo basi kufaulu inawezekana.

***2: Marafiki wabaya,*** mwanzoni nilikuwa sielewi ni kivipi marafiki wanaweza kuwa chanzo cha wanafunzi kufeli. Ila kwa sasa ninaamini kuwa urafiki mbaya unapelekea wanafunzi kutokufanya vizuri. Les brown anatolea ufafanuzi zaidi juu ya madhara yaliopo kwenye urafiki usio na tija kwa mfano wa nyanya nzima na nyanya mbovu anasema ukiwa na nyanya nzima tano na mbovu moja zikiwekwa sehemu moja yaani kwenye chombo kimoja kwa siku tatu nyanya nzima zilizokuwa karibu na ile mbovu moja zitaanza kuharibika,ndivyo hata kwenye kufaulu,mwanafunzi akiambatana na wanafunzi wenye tabia zisizopendeza na wao wanaathirika kama ilivyo kwenye nyanya.

***3: Tabia mbaya,*** hapa namaanisha tabia zote ambazo zinakinzana na utaratibu wa maisha wa kila siku na zile zinazokinzana na maadili ya uanafunzi. kinacholeta ufaulu mzuri ni tabia. Subira ni mwanafunzi wa kidato cha nne anayefanya vizuri sana darasani ilipofika mwezi wa sita baada ya mtihani wa mock alianza visa na vitimbwi. Kila siku alikuwa anapewa adhabu,basi hekaheka zilienda mpaka mwezi wa nane. Kufika mwezi wa tisa akastuka,akawa mpole akashuka chini,akatulia na kuanza kusoma,alisomasoma na mwisho wa siku aliishia kupata daraja la tatu badala ya daraja la kwanza zuri. Mzazi kamata nidhamu ya mwanao shirikiana vizuri na walimu wake.

***4: Mambo mengi,*** mwanafunzi mwenye mambo mengi ni ngumu kufanya vizuri katika masomo yake watu wengi husema ili mwanafunzi afaulu ni lazima afeli kwanza mambo ambayo hayana faida katika safari yake ndipo afanye vizuri darasani.

***5: Kukosa ratiba,*** kingine kinachomfanya mwanafunzi kutokufanya vizuri ni kukosa ratiba. Ratiba ndio uti wa mgongo wa wanafunzi, Mwanafunzi asiye na ratiba binafsi anaweza akawa anasoma somo moja ama mawili kwa wiki ama mwezi mzima na kushindwa kusoma masomo mengine.

***6: Kukosa mwendelezo,*** ili mwanafunzi aweze kushika na kuhifadhi alichokisoma anapaswa kuwa na mwendelezo wa kujisomea kila wakati.

***7: Kutokujijua,*** ipo namna hii mwanafunzi asiyejua ni njia ipi inawezakumsaidia kuelewa hataweza kufanya vizuri.

***8: Kutokufanya maswali mengi,*** tunaishi katika ulimwengu ambao unabadilika kila siku,zamani maswali yalikuwa ya moja kwa moja kiasi kwamba mwanafunzi akikomaa na notes anauwezo wa kufanya vizuri lakini sasa hivi bila kutafuta maswali ni ngumu

# ELIMU JAMII:

## ELIMU KWA WAZAZI NA WALEZI

sana kumudu kujibu maswali kwenye mtihani, usomaji uendane na ujibuji wa maswali.

***9: Mazingira,*** mazingira chanya huleta matokeo chanya, mwanafunzi akikosa mazingira mazuri ya kujisomea uwezekano



Mwl. Juliana Isondo. Soni Day Secondary

wa kufanya vizuri unakuwa mdogo,wazazi jitahidini kuwapatia watoto wenu mazingira tulivu ya kujisomea.

***10: Uvivu,*** wanafunzi wengi wanafeli kwa sababu ya uvivu wengi wao hawapendi kujisomea. Namkumbuka mwanafunzi wangu mmoja tumwite Halima aisee alikuwa anapenda sana kusoma siku ya mahafali yake alipokea zawadi kwenye masomo yote,na cha ajabu kesho yake asubuhi sana alikutwa darasani akiendelea kujisomea wakati wahitimu wenzake wakiwa wamelala na kufurahia zawadi walizoletewa.

***11: Kukosa ramani ya anakokwenda,*** wanafunzi walio wengi wanasoma ama wanaenda shule wakiwa hawajui sababu ya kwenda shule. Wengi wanakwenda shule kwa sababu wamefaulu hawajui kabisa faida ya kusoma wala ya kufaulu,hii inawafanya wasijisomee.

***12: Kutokujua asome nini ili awe nani,*** hii changamoto sijui niirushe kwa wazazi,wanafunzi ama walimu. Kwakuwa kuna msemo usemao elimu huanzia nyumbani naomba tu niirudishe kwa mzazi, mzazi unajukumu la kumsadia mwanao kufahamu asome nini ili awe nani hii itapunguza wimbi la wanafunzi wanaojiita madaktari na hawasomi fizikia na kemia.

***13: Kutokutimiziwa mahitaji,*** moja ya sababu inayowafanya wanafunzi kutokufanya vizuri ni ukosefu wa mahitaji mathalani madaftari,kalamu na mahitaji mengine muhimu. Namkumbuka mwanafunzi wangu mmoja anamadaftari manne ilhali anamasomo saba.

Anachokifanya sasa daftari moja anaandika masomo mawili kimbembe huja muda wa kufanya maswali marazote hushindwa kukusanya madaftari hayo kwa hofu ya kupewa adhabu.

***14: Kukosa msimamo,*** Msimamo ni muhimu sana kwa kila mwanadamu lakini zaidi sana kwa kila mwanafunzi,tuliopo mashuleni tunaona jinsi gani mwanafunzi asiye na msimamo anavyopelekwa/pelekeshwa na wenzake. Mwanafunzi asiye na msimamo maranyingi sana huamuliwa mambo mengi na wenzake. Hasa maswala ya kusoma.

**Usiache kunifuatilia facebook na instagram**
**JULIANA ISONDO**
**Soni Day Sekondari**
**Bumbuli Tanzania**
**0758463395**

## Tangazo




JAMVI la SIMULIZI

www.richardmwambe.com

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi

jamvilasimulizi@gmail.com